

**MAJI HUSHUKA MLIMA**

1. Waswahili walisema, ndugu wakituambia.  
Maji hushuka mlima, chini yakakimbilia.  
Yakenda hadi mrima, ndani kumiminikia.  
Kitu kule hutokea, kikaenda kwa jamaa.
2. Huacha kwenda kwa mama, mzazi alokulea.  
Kikaenda kwake mama, mama anokunyonyea.  
Na ndugu hufanywa kama, kitu kino najisia.  
Kitu kule hutokea, kikaenda kwa jamaa.
3. Na wengine walisema, uache kujivunia.  
Cha ndugu acha sakama, fakiri utajifia.  
Hayo waliyokalama, mimi ninawasifia.  
Kitu kule hutokea, kikaenda kwa jamaa.
4. Habibu nae kasema, ndugu bora zaidia.  
Huyo kwako mwanamama, leo ati mzuria.  
Kesho kitu kikihama, mwandani atakimbia.  
Kitu kule hutokea, kikaenda kwa jamaa.
5. Amekuumba Rahima, ewe mwana Adamia.  
Ujivalie makama, ukikalia gunia.  
Ndiyo wakufanya kama, punda asiye mkia.  
Kitu kule hutokea, kikaenda kwa jamaa.
6. Leo wakufanya nyama, kesho watakuijia.  
Wakikwita muadhama, shida wakikulilia.  
Wakiitaka hiitima, wende na kuwasomea.  
Kitu kule hutokea, kikaenda kwa jamaa.
7. Hata ukisha isoma, tabia watarudia.  
Kukuona kama kima, shida ukiwafutia.  
Pembeni wakikutema, ewe mwana Adamia.  
Kitu kule hutokea, kikaenda kwa jamaa.
8. Hayo niliyoyasema, ndugu yatakuijia.  
Lau silvyo yatahama, kwangu y atakimbilia.  
Ila utambue kama, cha akhi kitokujia.  
Kitu kule hutokea, kikaenda kwa jamaa.

*Hamidu R. Tambwe  
MBEYA,  
Desemba, 1967.*